## MASHARTI YA KUPATA LESENI YA BIASHARA

Mtu yeyote raia wa Tanzania anayo haki ya kupatiwa leseni ya biashara ili mradi awe ametimiza umri wa miaka kumi na nane (18) mwenye akili timamu ambaye hajawahi kupatikana na kosa la jinai na awe na eneo la kufanyia biashara linalokubalika kisheria.

Kwa mtu ambaye sio raia wa Tanzania anapaswa kuwa na kibali kinachomruhusu kufanya biashara nchini kutoka Idara ya Uhamiaji.

## UTARATIBU WA KUPATA LESENI YA BIASHARA

Mwombaji anapaswa kujaza fomu ya maombi 9TFN 2110 kikamilifu na kuambatanisha kivuli cha:-

(i) Jina la Biashara kama sio mtu binafsi (Certificate of Incorporation or Registration).

(ii) "Memorandum and Article of Allocation" kama ni Kampuni

(iii) Kitambulisho cha mpiga kura, Cheti cha kuzaliwa au Hati ya kiapo kuonyesha kuwa ni Mtanzania na Mgeni Hati ya kuishi nchini daraja la "A" (Residnece Permit Class "A").

(iv) Hati ya kiuwakili (prowess of a Honey) kama wenye hisa wote wa Kampuni wapo nje ya nchi.

(v) Ushahidi wa maandishi kuwa ana mahali pa, kufanyia biashara (Kwa mfano hati za nyumba, mkataba wa upangishaji, risiti za malipo ya kodi za majengo au ardhi.

(vi) Hati ya kujiandikisha kama mlipa kodi TRA (TIN).

Kwa leseni zinazodhibitiwa na Mamlaka mbalimbali , Kwa mfano (TFDA, EWURA, TAURA, CRB, TILLI) n.k lazima mwomaji kuwa na leseni husika kablaya kuomba leseni ya biashara fomu ya maombi ya biashara (TFN 211) hutolewa kwa ada ya Tshs. 1,000/=.

Baada ya kujaza fomu na viambatanisho, maombi hupitishwa ngazi zinazotakiwa kisheria – Mpango Miji na Afya. Baada ya hapo leseni hutolewa ndani ya siku moja au mbili na si zaidi.

Angalizo: Kwa utaratibu wa kuanzia mwaka 2004/2005 leseni mpya hutolewa bila malipo ya ada za leseni na leseni zote hutolewa mara moja tu hadi sheria mapya (BARA) itakapoanza kutumika.

**MASHARTI YA UTUMIAJI WA LESENI**

1. Mwenye leseni hataweka masharti yeyote kwa mnunuzi.

2. Mwenye leseni atatoa risiti kwa mauzo yote.

3. Mwenye leseni atafuata sheria ya leseni ya Biashara No. 25 ya 1972.

4. Mwenye leseni hatapewa huduma/bidhaa amao hazizingatii viwango vya ubora,uliowekwa na vyombo vinavyotumika kisheria.

5. Mwenye leseni anaweza kunyaganywa wakati wowote ikiwa itaonekana aliipata kwa njia ya danganyifu au amekiuka msharti ya leseni.

**MAKOSA**

i. Kuendesha biashara bila leseni.

ii. Kuendesha biashara eneo tofauti na linaloonyeshwa kwenye leseni.

iii. Kutumia leseni moja kufanyia biashara zaidi ya moja au maeneo mawili au zaidi.

iv. Kushindwa kuonyesha lesenid ya biashara inapotakiwa kufanya hivyo na Afisa aliyeidhinishwa na Serikali.

v. Kutokuweka leseni ya biashara mahali ambapo inaonekana kwa urahisi.

vi. Kutoa maelezo ya uongo ili kupata leseni au kukwepa kulipa ada/kodi inayostahili.

vii. Kumzuia Afisa wa Serikali aliyepewa mamlaka ya kukagua kufanya kazi yake.

**ADHABU**

Mtu yeyote anayetenda majawapo ya makosa hapo juu adhabu yake ni faini isiyopungua Tshs. 50,000/= na isiyozidi Tshs. 100,000 au kifungo kisichozidi miaka miwili (2) au faini na kifungo kwa pamoja.

## LESENI ZA VILEO

Sheria ya leseni za vileo imenyambulisha aina tisa za leseni za vileo zinazoweza kutolewa chini ya sheria hii:

Retailers On
Leseni hii humruhusu mwenye biashara kuuza pombe na kunywa eneo la biashara

## RETAILERS OFF

Leseni hii haimruhusu mtu kinywea pombe eneo la biashara bali kwa watu wanaochukua kunyewea majumbani (Take away) kama Groceries.

## WHOLESALE

Leseni hii ni kuuza pombe kwa jumla

## HOTEL

Leseni hii humruhusu mwenye leseni kuuza pombe kwa ajili ya kunywea katika eneo la biashara kwa watu waliopanga hotelini kwa wakati wowote wa mchana na usiku

## RESTAURANT

Leseni hii inamruhusu mwenye leseni kuuza pombe kwa mtu yeyote anayekula chakula katika mgahawa katika muda wa saa 6.00 mchana hadi saa 8.00 mchana na saa 12.00 hadi saa 6.00 usiku.

## MEMBERS CLUB

Leseni hii huruhusu uuzaji wa pombe kwa kiasi chochote kwa mwanachama wa Klabu na wageni wao tu

## COMBINED

**Leseni ambazo zimeambatanishwa mhili kwa pamoja:**

(a) Combined Hotel and retailers on
(b) Combined Hotel and Restaurant
(c) Combined restaurant and retailers on

**TEMPORARY**

Leseni hii humruhusu mwenye leseni kuuza pombe katika sehemu iliyotajwa kwenye leseni mahali penye burudani, starehe au mkusanyiko mwingine kwa kipindi kisichozidi siku tatu

**LOCAL LIQUOR**

**Class A Local Liquor**
Leseni hii humruhusu mwenye leseni kutengeneza pombe za kienyeji katika sehemu iliyotajwa na kuuza kwa ajili ya kunywea sehemu ya biashara au nje ya sehemu ya biashara

**Class B Local Liquor**
Leseni hii humruhusu kutengeneza pombe ya kienyeji sehemu iliyotajwa na kwenda kuuzia sehemu nyingine iliyo na leseni ya kuuza pombe za kienyeji

**Class C Local Liquor**
Leseni hii humruhusu kutengeneza pombe ya kienyeji katika sehemu iliyotajwa kwenye leseni na kuuza kwa mwenye class D au Class E

**Class D Local Liquor**
Leseni hii humruhusu kuuza pombe za kienyeji katika sehemu iliyotajwa kwenye leseni kwa kunywea eneo la biashara

**Class E Local Liquor**
Leseni hii humruhusu kuuza pombe za kienyeji kwa ajili ya kunyewea sehemu nyingine mbali ya eneo la biashara

1. **MASHARTI YA KUPATA LESENI**

Mtu yeyote raia wa Tanzania anayo haki ya kupatiwa leseni ya

Vileo ili mradi awe ametimiza umri wa miaka kumi na nane (18) mwenye akili timamu ambaye hajawahi kupatikana na kosa la jinai na awe na eneo la kufanyia biashara linalokubalika kisheria.

Kwa mtu ambaye sio raia wa Tanzania anapaswa kuwa na kibali kinachomruhusu kufanya biashara nchini kutoka Idara ya Uhamiaji.

## 2. UTARATIBU WA KUPATA LESENI

- Mwombaji hujaza fomu za maombi zinazotolewa na Manispaa
- Eneo/jingo linalokusudiwa kufanyia biashara hiyo kukaguliwa na Afisa Afya, Afisa Mipangomiji, Polisi, Afisa Mtendaji wa Kata (WDC) na Afisa Biashara wa Manispaa na hutoa maoni yao kwenye fomu husika
- Maombi hayo hupelekwa katika Malaka ya Utoaji wa Leseni za Vileo ya Manispaa kwa uamuzi
- Mwombaji ambaye maombi yake yamepitishwa hupewa Leseni baada ya kulipa ada inayotakiwa na ni lazima amekamilisha masharti ya kupata leseni hapo juu

## VIWANGO VYA ADA

Viwango vya ada vinavyotumika kwa sasa kwa aina mbalimbali za leseni ni kama zifuatavyo:-

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Retailers On (Baa) | - 30,000.00 | hadi | 40,000.00 |
| 2. | Retailers Off (Grosari) | - 20,000.00 | hadi | 30,000.00 |
| 3. | Wholesale (Jumla) | - 10,000.00 | hadi | 20,000.00 |
| 4. | Members Club (Klabu Wanachama) | - 10,000.00 | hadi | 20,000.00 |
| 5. | Restaurant & Retailers On | - 30,000.00 | hadi | 40,000.00 |
| 6. | Temporary licence (Leseni ya muda) | - 7,000.00 | hadi | 15,000.00 |
| 7. | Hotel Licence (Leseni ya Hoteli) | - 30,000.00 | hadi | 40,000.00 |
| 8. | Retailers Off non-spirituous | - 7,000.00 | hadi | 15,000.00 |
| 9. | Retailers On – non-spirituous | - 10,000.00 | hadi | 15,000.00 |

Mamlaka ya Vileo itaamua kiwango cha ada kitakachotozwa kati ya kiwango cha chini na kile cha kima cha juu. Viwango vinavyotumika kwa sasa na Manispaa ni vile vya kima cha juu kwa kila aina ya leseni.

## 3. MASHARTI YA UTUMIAJI

Leseni za vileo zina masharti mengi ikiwa ni pamoja na kutouza kilevi

kwa watoto. Masharti mengine ni muda wa kuuza pombe na kelele za muziki.

**MUDA WA KUUZA POMBE**

**BAA (RETAILERS ON)**

- Jumatatu hadi Ijumaa - Saa 12.00 jioni hadi saa 5.00 Usiku
- Jumamosi, Jumapili na Sikukuu - Saa 5.00 asubuhi hadi saa 8.00 mchana na saa 12.00 jioni hadi saa 6.00 usiku

**GROSARI (RETAILERS OFF)**

- Jumatatu hadi Ijumaa - Saa 2.00 asubuhi hadi saa 1.00 jioni
- Jumamosi, Jumapili na Sikukuu - Saa 3.00 asubuhi hadi saa 6.00 mchana

**RESTAURANT LICENCE (MGAHAWA)**

- Jumatatu hadi Ijumaa - Saa 6.00 mchana hadi saa 8.00 mchana na saa 12.00 jioni hasi saa 6.00 usiku
- Jumamosi, Jumapili na Sikukuu - Saa 5.00 asubuhi hadi saa 8.00 mchana na saa 12.00 jioni hadi saa 6.00 usiku

**MAKOSA**

Baadhi ya makosa chini ya sheria hii:

- Kuruhusu biashara nyingine isiyokubalika kisheria kufanyika eneo la biashara
- Kuuza pombe kwa mtu mwenye umri chini ya miaka kumi na sita (16)
- Kuajiri mtu chini ya miaka kumi na sita (16) kuuza pombe
- Kuruhusu mtu mwenye umri chini ya miaka kumi na sita kukaa eneo la kuuzia pombe
- Kutoweka leseni sehemu ya wazi, ambapo itaonekana kwa urahisi na wakaguzi
- Kumruhusu/kuleta fujo katika eneo la biashara
- Kuruhusu eneo la biashara kutumika kama danguro
- Kuuza pombe muda ambao ni kinyume cha sheria
- Kufanya biashara ya pombe kwa kutumia leseni ya vileo ambao haistahili

**ADHABU**

Mfanyabiashara anayetenda mojawapo ya makosa haya akikamatwa, atafikishwa mahakamani na akitiwa hatiani atalipa faini au kifungo au adhabu zote kwa pamoja.

**II UTARATIBU WA USHURU WA MALAZI (HOTEL LEVY) CHINI YA SHERIA NA. 23 YA 1972**

**MASHARTI YA KULIPIA HOTEL LEVY**

1. Kila mmiliki wa nyumba ya wageni (Guest House) anapaswa kulipa kodi ya asilimia ishirini (20) ya malipo ya nyumba (Guest House charges) kwa mwezi husika. Wamiliki wenye mauzo yanayotozwa kodi ya zaidi ya Tshs. 40 milioni kwa mwaka hawatalipa kodi ya malazi bali watalipa Kodi ya ongezeko la tghamani (VAT)

2. Kodi iliyowekwa, italipwa kuanzia tarehe moja hadi tarehe saba ya mwezi unaofuata mauzo

**UTARATIBU WA KULIPIA HOTEL LEVY**

- Malipo ya Ushuru wa Malazi ni lazima yaambatanishwe na fomu ya mapato ya kila siku (fomu H.L. 1) au kitabu cha wageni, na fomu ya mapato ya kila mwezi (fomu H.L.2)

- Mmiliki wa nyumba analeta fomu H.L.1 au kitabu cha wageni pamoja na fomu H.L. 2 ambaye amekwisha jaza. Afisa anayekadiria atapitia H.L.1 au kitabu cha wageni na fomu H.L. 2 ili kuhakikisha ni sawa na kuhakikisha mmiliki amefikia vizuri asilimia 20 ya mapato ya malazi ya mwezi.

- Mmiliki akishindwa kulipa ushuru kwa muda uliopangwa, siku saba (7) baada ya mwezi husika kumalizika, atalipa nyongeza ya asilimia 25 ya ushuru unaotakiwa kulipwa, na endapo ataendelea kutokulipa adhabu (penalty) itakuwa inaongezeka kwa asilimia kumi (10) ya ushuru uliotakiwa kulipwa kila baada ya siku thelathini (30) kumalizika

**MAKOSA**

- Mmiliki wa nyumba ya kulala wageni kushindwa kulipa ushuru wa malazi kwa muda unaotakiwa

- Kushindwa au kukataa kuwasilisha fomu ya mapato ya kila mwezi

- Kushindwa kuweka na kutunza kitabu chenye kumbukumbu sahihi za kulala wageni

- Kushindwa kutoa risiti, hati za madai na kumbukumbu nyinginezo kama sheria inavyotaka

- Kumzuia Mkurugenzi au Mwakilishi wa Mkurugenzi katika kufanya kazi zake zilizowekwa na sheria au Kanuni za Ushuru wa Malazi

- Kushindwa kutekeleza Ilani iliyotolewa na Kamishna/mkurugenzi ya kuitwa na kuwasilisha nyaraka zinazohusu nyumba yake ya kulala wageni

- Kutoa taarifa ya uongo kwenye kumbukumbu yeyote inayotumika kwa ajili ya kudanganya au kushindwa au kukataa kujibu maswali vizuri kwa Afisa wa Serikali aliyepewa madaraka na sheria hii

## ADHABU

- Mmiliki atakayetenda mojawapo ya makosa yaliyotajwa hapo juu atalipa faini isiyopungua Tshs. 50,000.00 kwa Mkruugenzi wa Manispaa na isiyozidi Laki tano (500,000.00) Mahakamani akipatikana na hatia.

- Mmiliki anayekwepa kulipa Ushuru wa Malazi kwa makusudi akikamatwa na kutiwa hatiani atalipa faini isiyozidi shilingi milioni mbili (2,000,000.00)

## IV (i) **USIMAMIZI WA BIASHARA NDOGO NDOGO**

## HALMASHAURI YA MANISPAA YA TEMEKE

# TANGAZO

## UTOAJI WA LESENI ZA VILEO KIPINDI CHA KUANZIA TAREHE 01.10.2010 HADI 31.03.2011

**(Chini ya Sheria ya Leseni za Vileo Na. 28 ya 1968 na marekebisho yake)**

Wafanyabiashara wote wanaoendesha biashara ya Vileo katika Halmashauri ya Manispaa ya Temeke wanatangaziwa kwamba, leseni za Vileo kwa kipindi kitakachoanza tarehe **01.10.2010** hadi **31.03.2011**, zinaanza kutolewa kuanzia tarehe **01.10.2010.**

Fomu za maombi ya Leseni za Vileo, zinapatikana katika Ofisi ya Mkurugenzi wa Manispaa ya Temeke, Makao Makuu ya Manispaa iliyoko karibu na Uwanja wa Taifa na barabara ya Mandela.

Fomu za maombi mapya na ya zamani, zijazwe kikamilifu na kurejeshwa sehemu ya Biashara na viwanda Manispaa ya Temeke kabla ya tarehe **20.9.2010.** Fomu ya maombi yanayorudiwa (Renewal) iambatishwe na kivuli (Photocopy) cha leseni ya kipindi kinachoishia tarehe **30.09.2010.**

**MWISHO:**

**(i) Mamlaka ya Utoaji wa Leseni za Vileo ya Halmashauri ya Manispaa ya Temeke, haitahusika kwa lawama yeyote itakayotolewa na mwombaji aidha kwa kuchelewesha ombi lake, au kwa kutokuzingatia tarehe ya mwisho ya uwasilishaji wa maombi.**

**(ii) Ieleweke pia kuwa, hatua kali za kisheria zitachukuliwa dhidi ya yeyote atakayekutwa akiendesha biashara ya vileo bila ya leseni halali ya kipindi/vipindi husika.**

**(iii) Wafanyabiashara wanatahadharishwa kutokuwatumia mawakala au watu wasiohusika katika kushughulikia masuala ya leseni zao, kutokana na udanganyifu wanaoufanya wa kudai malipo yasiyokuwepo au kutoa taarifa za uongo.**

**STEPHEN M. KONGWA**
**MKURUGENZI WA MANISPAA**
**TEMEKE**

Uendedhaji wa biashara ndogondogo unasimamiwa na sheria ndogo ya Jiji ya mwaka 1991 (The Dar es Salaam City Town/(Hawking and Street trading) amendment By – law 1999) sheria hii inalenga kuthibiti uharibifu wa Mazingira, kuhatarisha maisha/Afya za wananchi, kuleta sura mbaya ya Mji na uvamizi wa maeneo ya wazi/starehe.

**MASHARTI YA KUFANYA BIASHARA**

- Mfanyabiashara awe safi na nadhifu
- Umbo chombo safi cha kufanyia biashara
- Eneo la kufanyia biashara
- Kuboreshad na kuhifadhi mazingira
- Kuwe na eneo la kufanyia biashara linalokubalika kisheria

**UTARATIBU**

Manispaa imetenga maneo ya Tazara (RTD), Tandika (Kamochea), Rangitatu, Charambe, Temeke Stereo na Tandika Sokoni kwa ajili ya wafanyabiashara ndogondogo.

**MAKOSA**

Sheria hii ndogo inamzuia mtu kufanya biashara kwenye maeneo yafuatayo:-

- Bustani za Jiji /Manispaa

- Mbele za nyumba za Serikali, Taasisi za Fedha, Ofisi za Ubalozi, Mashirika ya Serikali, Kimataifa, Nyumba za Ibada na Taasisi zisizo za Kiserikali (NGOs).

- Mashule, Hospitali, Maeneo yaliotengwa kwa kumbukumbu za Kitaifa.

- Maeneo yanayozuia mtu kuingia na kutoka kwenye jingo.

- Maeneo yenye kumzuia au kuleta usumbufu kwa watembea kwa miguu.

- Maeneo ya kupumzikia (bus stand) au kuegesha magari.

- Kutundika bidhaa kwenye majengo ya watu, Taasisi, Miti, Kuta (Fence) nguzo za taa, Umeme, vituo vya simu, viti vya kumpumzikia wasafiri.

- Kutembeza bidhaa Maofisini.

**ADHABU**

Mfanyabiashara atakeyetenda majawapo ya makosa haya akikamatwa atafikishwa Mahakamani na adhabu yake ni  faini au kifungo au vyote kwa pamoja.

Usajili wa Taxi Cabs chini ya Sheria ndogo ya Jiji (The City of Dar es Salaam (Registration of Taxi –cabs and Private Hire Vehicles) By-law, 1968

**MASHARTI**

Mmiliki wowote wa gari ndogo anayetaka kusajili gari lake ni lazima akamilishe masharti yafuatayo:

- Rangi ya gari iwe nyeupe
- Iwe imechorwa mstari wa bluu ubavuni
- Iwe imekaguliwa na Polisi wa Usalama barabarani na ripoti ya ukaguzi iwe imekamilika
- Mmiliki awe amekwisha lipia tozo zote za Mamlaka ya Mapato na kupewa stika na leseni ya taxi (sticker and Taxi =-cabs licence) kutoka TRA

**UTARATIBU**

Mwombaji anatakiwa kufika na kivuli cha Kadi ya gari na awe ametimiza masharti yaliyotajwa.  Atapewa fomu ya maombi ya usajili na atajaza kikamilifu na kuambatanisha:

- Kivuli cha Kadi ya gari
- Ripoti ya ukaguzi
- Stika kutoka Mamlaka ya Mapato
- Taxi – cab licence kutoka Mamlaka ya Mamlaka ya Mapato
- Kituo cha kuegesha

Mmiliki baada ya kukamilisha taratibu atalipa ada ya Tshs. 61,000.00 kwa mchanganuo ufuatao:

- Ada ya Maegesho - Tshs. 36,000.00
- Ada ya Usajili - Tshs. 20,000.00
- Ada ya Kituo - Tshs. 5,000.00

**JUMLA - Tshs. 61,000.00**

Baada ya malipo anapata Hati ya Usajili na namba ya ubavuni.

**MAKOSA**

- Kufanya biashara ya taxi-cabs bila ya kusajili
- Kuegesha Taxi – cab kwenye Kituo ambacho hakijaainishwa
- Kutokuwa na ripoti ya ukaguzi ya Polisi wa Usalama barabarani
- Kutokuwa na Leseni ya Taxi-caba
- Kutokuwa na Stika

**ADHABU**

Anayefanya kosa lolote atakamatwa na Mamlaka inayohusika na kufilishwa kwa kosa hilo.